# Nitakuwa na furaha kama...
## nitamlinda Mungu ndani yangu na ndani ya wengine

Heri wenye moyo safi, maana watamwona Mungu (Mt. 5,8)

### Ndani ya maneno

Moyo: kwa wayahudi moyo ni kiini cha hisia, mawazo, nia za mwanadamu. Sisi tunaweza kumwona Mungu kwa kupitia moyo wetu kwa sababu unajumuisha utu wa mwanadamu katika uwezo wake wa kupenda na kupendwa.

Msafi wa moyo: ni yule aliye na nia ya kumtazama Mungu moyoni mwake, katika dhamira yake, jinsi alivyo na ndugu zake jinsi walivyo.

### Lengo

- Kutambua kwamba uhusiano wetu na Mungu ni kitu cha thamani cha kukilinda.
- Kujifunza zaidi dhana ya usafi katika mahusiano ya kibinadamu na kuukubali mtindo wa maisha unaoheshimu hadhi na uhuru wa mtu.

### Mambo yaliendaje?

Mwanzoni kuna sehemu ya makaribisho, ambapo inabidi kuacha nafasi ya mazungumzo na mawasilisho ya kile ambacho kila mtu ameishi, mang'amuzi na magumu pia. Kukaribisha maana yake ni kumfanya kila mtu ajisikie nyumbani: ubunifu utatusaidia kupata mbinu zinazofaa. Pia tunaweza kujikumbusha malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa mwisho: "ulikuwaje?"



### Shughuli ya utambulisho

**AINA:** kazi ya picha za kidigitali

**MUDA:** ni vizuri kuchukua lisaa limoja, mwishowe makundi yapewe muda wa kutosha ili kumalizia kazi.

**VIFAA:** kamera za kidigitali au simu za mkononi, makaratasi makubwa, kalamu za rangi tofauti tofauti, mikasi, printer.


**UTEKELEZAJI:** kundi ligawanyike katika makundi madogo kama ni lazima. Idadi inayofaa ili kazi ifanyike ni ya watu watano au sita. Waombe vijana wafikirie na wapige picha zinazowawakilisha walio na usafi wa moyo pamoja na mahusiano yao. Hizo picha zitachapishwa na kukatwa halafu zitambandikwa kwenye karatasi kubwa. Waombe watafute kichwa cha habari kinachofupisha maana ya hii heri. Vijana wanaweza kuweka sahihi zao juu ya hilo karatasi kubwa, kama alama ya uanachama wa mfano kwa heri iliyopendekezwa. Uwezekano mwingine wa toleo lilichapishwa, vijana wanaweza kutengeneza 'Power Point'. Licha ya wao wenyewe kupiga picha, wanaweza kutafuta kwenye 'internet' picha au nukuu zinazofaa.

Ni muhimu kutilia mkazo kwamba kuwa wasafi na kuishi usafi hakuhusu mambo ya ngono tu bali maisha yetu yote. Ni namna ya kufikiri na kuyaona mahusiano yetu ( na wengine na pia na Mungu) hii inatufanya tuwe makini katika uhuru wetu na hadhi yetu na ya wengine.

Kazi ya kubuni ikikamilika kila kikundi kinaweza kuonesha matokeo ya kazi yake, kwa kutoa sababu ya uchaguzi wa picha, wa kichwa cha habari na mwishowe wa maneno yaliyowekwa kwenye karatasi au PPT.

**HITIMISHO:** acha nafasi ya mazungumzo. Hapa kuna baadhi ya maswali ya mfano: kuna kitu tulichoelewa na tungependa kushirikishana na wote? Kitu gani kilionekana kuwa kigumu au kilichotupatia furaha? Ni changamoto gani tunaziishi kila siku katika kutekeleza heri hii?

# Tuishi hivi



## Katika njia panda moja

Siku zote nilipenda sana uhuru ambao kwangu ilimaanisha kufanya ninachopenda. Ninapenda sana kuteleza juu ya barafu, na wakati wa likizo ya kiangazi nilikuwa nabaki kileleni siku nzima. Kundi la marafiki niliokuwa nateleza nao liligawanyika, walikuwa wanaongeleshana vibaya na hali ya mahusiano ilibadilika sana. Walianza hata kunywa na kutumia madawa ya kulevya. Wangine walikuwa wanakunywa sana kiasi cha kutoweza tena kusimama kwenye mtelezo. Na wengine walikuwa wamelewa daima, walikuwa wakigombana na watu wote.

Mimi sikuwa nimeanza kunywa bado, lakini naamini kuwa nisingehimili kwa muda mrefu. Siku moja mama wa mvulana mmoja alipogundua, alikuja nyumbani kwangu kumwambia mama yangu. Walipokuwa wanaongea, nilijifungia chumbani kwangu. Nilitambua kuwa nilikuwa nimefuata njia mbaya: ningeendelea hivi ningeishia pabaya. Nilikuwa katika njia panda na nilitakiwa kufanya uchaguzi: kuwafuata wale marafiki au kumfuata yule rafiki mwingine, Mungu. Niliamua kuacha mazingira yale. Mchezo wa kuteleza ulibaki kuwa hamu yangu kubwa, lakini sasa sijiachii nishawishike tena na ninajisikia kuwa huru kweli.

*(N. - Olanda)*

## Hapana kwa tv dicteta

Athari ya tv ilianza kupenya hata katika familia yangu. Kati yetu ndugu tuliokuwa tumeanza kung'amua kutowajali wengine, tulikuwa tunagombana mara nyingi, tulikuwa tunafanya vibaya shuleni na tulikuwa tunaigiza mamodo kwenye televisheni. Tulipoongea na mama na baba, tuligundua kuwa tv ilitufanya kuwa watumwa, na hasa hatukuwa na furaha: zile jumbe za uongo zilikuwa zinatushurutisha kuzima upendo ndani yetu. Wazazi wetu walitushauri tusiangalie televisheni kwa mwezi mmoja: ulionekana kuwa uwezekano pekee wa kurudi kuwa na moyo safi. Sote tulikubaliana tukaweka televisheni ndani ya kabati na kufunga. Mwanzoni haikuwa rahisi, kwa sababu yalikuwa mazoea mabaya kuangalia televisheni kila wakati usio wa kazi, lakini uhusiano ndani ya familia ukawa mzuri zaidi. Tulikuwa tunaongea zaidi, tulikuwa tunaenda kutembea pamoja, tulikuwa tunafanya maonesho ya ghafla, tulikuwa tunaenda kuwatembelea marafiki, tulikuwa tunabuni michezo na mmoja wetu alijifunza kupika alipokuwa akimsaidia mama. Ili kupata habari mpya tulikuwa tunasoma gazeti au kusikiliza redio. Alama za wote shuleni zikaongezeka. Tulipoanza kupiga hesabu ya tangu tulipoacha kuangalia televisheni, tuligundua kuwa ilikuwa imepita miaka miwili: tulipona kabisa! Sasa tv imerudi mahali pake: mara moja moja huiwasha na kuangalia kwa pamoja, lakini kama kuna programu nzuri tu.

*(P. - Brasile)*

Kwangu ilitokea...

## Kwa undani

# FURAHIA KUWA NA MUNGU



***Chiara Lubich,*** *Kongamano la gen 3, Heri, 20 June 1975*

Kama kijana mmoja hana moyo wa kweli, kama hataki kufanya matakwa ya Mungu badala ya matakwa yake, kama mabaya mengi yamejaa moyoni mwake, ni wazi kwamba hawezi kumwona Mungu.

Yesu anasema wana heri walio na moyo safi, yaani wale wanaolinda moyoni mwao mawazo ya upendo, huruma, usafi, ukweli, kutong'ang'ania vitu ambavyo ni kizuio cha kumfuata Yesu na amri za Mungu. Tumtazame Bikira Maria. Yeye ni kiumbe aliye na usafi wa moyo ulio bora kabisa, hakuwa na matarajio binafsi ndani yake, hakung'ang'ania vitu wala miradi yake, bali mapenzi ya Mungu tu. Na sasa huko mbinguni hamuoni tu Mungu mwenye utukufu mkuu, bali katika maisha yake hapa duniani, Mungu alitwaa mwili wake na wakaishi katika nyumba moja. Hivyo watakatifu wengi, wasichana na wavulana wengi wanaojitahidi kutunza usafi wa moyo, wanasikia waziwazi ukaribu wa Mungu. Hawamuoni kwa macho, kwa sababu Yeye ni Roho tu, bali wanatambua sauti yake inayowaongoza, upendo wake katika yale yanayotokea, na katika magumu wanafurahia uwepo wake.

*Dokezo: kwenye wavuti http://assistentigen3.focolare.org pia video inapatikana*

## USIKATE TAMAA KAMWE

*Mara nyingi tunajikuta katika hali za uchungu, na ndugu zetu au rafiki zetu wanaolewa, wanavuta sigara, wanatumia dawa za kulevya au wanashiriki katika makundi mabaya; wakati mwingine wanatuogopesha au kutucheka kwa sababu hatupo kama wao; au kwa sababu hatuna 'boy friend'. Tupo katika ugumu wa kuishi kinyume cha mkondo... unayo siri ili tusikate tamaa? Tunawezaje kurudisha ile hadhi ambayo Mungu anaitaka kwa mwamke, katika mazingira yetu ambapo bado mwanamme hutawala mwanamke?*



**Siri ili kukaa katika dunia hii iliyo kinyume ni kuishi Upeo na kushikamana na wanagen wengine na Opera nzima, ambamo sasa utamaduni mpya unaundwa. Anayeishi utamaduni huu hata kata tamaa kamwe. Ili kurudisha hadhi kwa mwanamke inabidi kuishi Upeo ili kuwa Maria mdogo wa Guadalupe, yeye ambaye ni mwanamke anayependwa sana na wote.**

***Chiara Lubich,*** *Mji wa Mexico, 8.6.1997 – Majibu kwa jumuiya, n°4*


## KUMRUDISHA MUNGU KUWA FASHENI



***Chiara Lubich,*** *Rocca di Papa, 27.3.1976 – Kongamano la viongozi wa gen 3, n°3*

Sisi ni lazima tueneze mapinduzi yetu duniani, ambayo ni mapinduzi ya kweli, kwa sababu dunia nzima inaenda kinyume. Mambo yote mabaya yamekuwa mtindo wa kisasa nanyi mnajua. Ni lazima tumfanye Mungu arudi kwenye fasheni, wema urudi kwenye fasheni, usafi urudi kwenye fasheni, fadhila zote zirudi kwenye fasheni, vyote kwenye fasheni, kama mlivyozirudisha heri kwenye fasheni, ambako walikuwepo hata walio na usafi wa moyo. Basi na tuanze kumfanya Mungu awe fasheni.

Ni lazima tuombe msaada, wa Yesu kati yetu, ili kuona ni mwelekeo gani tunapaswa kuufuata ili kuupenyeza huu mtindo, mtindo huu mpya ambao sasa haupo lakini ambao kwa njia ya wanagen, utakuwapo.



## Nitajaribu!

Tunawezaje kuishi “ usafi wa moyo” wakati vitu vingi vinavyotuzunguka (matangazo, vyombo vya habari...) mara nyingi vinatupatia mtindo wa maisha uliokinyume? Kwa njia ya kubadilishana mawazo tutafute jukumu la kulifanya katika kipindi kijacho. Hapa kuna baadhi ya mifano:

- Nitajitahidi kutumia **dakika 10 kila siku kwa ajili ya uhusiano wangu na Mungu** kwa kusoma Injili (*), neno la Uzima au kwa kusali tu. Nitaandika katika daftari matukio, mang’amuzi yaliyonifanya nihisi upendo wa Mungu kwangu na nitashirikisha kwenye mkutano ujao.

  (*) Mapendekezo ya vifungu vya Injili vinavyohusu heri:
  Lc 11, 34-36; Gv 15, 1-11; Rm 13,11-14

- Nitakuwa makini “kumwona” Mungu ndani ya wengine na kuwatendea kwa heshima watu ninaokutana nao.



## Tupo katika hatua gani?

*Ili kulifikia **lengo ni lazima** kufanya mazoezi kila siku na kutambua mabadiliko mazuri na magumu yaliyojitokeza. Itatusaidia hadi katika mkutano ujao, tutakapotenga muda wa kushirikishana mang’amuzi.*

Nimesikia ukaribu wa Mungu katika maisha yangu, kwa yale yote yanayonipata, uongozi wake katika changamoto ninazokutana nazo?

Katika hali gani?

Hali yangu ya ndani ilikuwaje?

Kitu gani kilinisaidia kuhisi ukaribu wa Mungu?

**Kwa ajili ya mlezi**

## Tathmini baada ya mkutano

- Shughuli zilizopendekezwa zilikuza mvuto wa vijana kwa hii heri?
- Kuna eneo la pekee lililojitokeza ambalo gen 3 wanaona kuwa ni vigumu kutekeleza usafi wa moyo?
- Walichukua dhamira gani ili kuiishi? Lengo liwe kuwaongoza na kuwasaidia katika pendekezo lao hadi mkutano ujao.
- Nafikiri kuwa mada imekamilika au nadhani kuwa kuna kitu kinachokosekana cha kukijadili katika mkutano ujao?
- Kuna magumu yaliyojitokeza? Ni kitu gani cha muhimu kukumbuka ili kuboresha wakati ujao?